# ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P.O.BOX 14167
ARUSHA
**TANZANIA**
**TEL:** +255272970304
Mob: +255734026767
**E-mail:** arushameatcompany@yahoo.com


**KUMB. NA. AMCL/MTNZ/78/72** **DATE: 11/06/2025.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenye sifa kujaza nafasi tatu (3) zilizowazi kama ifuatavyo:Tangazo hili kwa nafasi mbili ya Meneja Fedha na Mtunza Stoo zimerudiwa kutangazwa kwa sababu mbalimbali.

## 1.0 MHASIBU (ACCOUNTANT) NAFASI MOJA (1).

### 1.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO;-

i) Kushiriki kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya mwezi.
ii) Kushiriki kuandaa hati za malipo na hati za mapokezi.
iii) Kuandaa taarifa mbalimbali za mishahara.
iv) Kushiriki kufanya usuluhisho wa hesabu za benki na nyingine zinazohusiana na masuala ya fedha.
v) Kusimamia kazi za wasaidizi wa hesabu.
vi) Kuandaa taarifa ya maduhuri.
vii) Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na mkuu wa kazi.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

i) Awe na shahada ya uhasibu kutoka taasisi yoyote inayotambuliwa na serikali.

ii) Mwenye cheti cha taaluma ya uhasibu CPA (T) au sifa inayolingana nayo inayotambuliwa na NBAA atapewa kipaumbele.

iii) Awe na uzoefu usiopungua mwaka (1) katika fani ya uhasibu.

**MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Company limited yaani ngazi ya **AMC 7.**

**1.1. MTUNZA STOO (STORE-KEEPER) NAFASI MOJA (1) - READVERTISED.**

**1.2. MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

i. Kuandaa na kutunza kumbukumbu zote za vifaa/bidhaa zinazoingia orodha /mtiririko (stock movement).
ii. Kuhakikisha stoo ipo katika hali ya usafi na mpangilio sahihi wa vifaa.
iii. Kutoa vifaa kutoka stoo kwenda kwa watumiaji kwa kuzingatia utaratibu ulioidhinishwa.
iv. Kupokea na kukagua ubora wa bidhaa/vifaa vinavyoingia kwa ajili ya matumizi mbali-mbali ya Kampuni.
v. Kupitia mara kwa mara mahitaji ya malighafi/vifaa kulingana na mahitaji na kutoa taarifa kwa Mkuu wa idara husika ili kuhakikisha uwepo wa mali ghafi/vifaa vya kutosha.
vi. Kuandaa na kutunza taarifa za manunuzi ya vifaa na malighafi ya manunuzi mbali-mbali.
vii. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za vifaa/malighafi zilizopokelewa stoo.
viii. Atawajibika kutekeleza Majukumu mengine atakayopangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**1.3. SIFA ZA MWOMBAJI.**

a) Awe na astashahada katika Manunuzi na Ugavi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali au Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) "Foundation stage I and II".
b) Mwenye uzoefu usiopungua mwaka mmoja (1) katika fani hiyo atapewa kipaumbele.
c) Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta.

**1.4. MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMC 1.**

**2.1. MENEJA FEDHA (ACCOUNTING AND FINANCE MANAGER)**

**NAFASI MOJA (1) - READVERTISED.**

**2.2. MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

i) Kumshauri Meneja Mkuu katika masuala yote ya fedha.

ii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Kampuni pamoja na kuhakikisha fedha zote zilizokusanywa zinapelekwa Benki kwa wakati na nyaraka zake zinatunzwa katika mazingira salama.

iii) Kuandaa bajeti ya mwaka ya Kampuni kwa kushirikiana na wakuu wa Idara wote pamoja na Meneja Mkuu.

iv) Kushirikiana na Meneja Mkuu kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuviboresha vyanzo vilivyopo kwa ajili ya uendeshaji wa Kampuni.

v) Kuratibu na kusimamia matumizi ya fedha kwa kuzingatia bajeti ya Kampuni iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi kwa mwaka husika wa fedha.

vi) Kuhakikisha Kampuni inalipa kodi mbalimbali za Serikali kwa mujibu wa sheria na taratibu kwa kushauriana na Meneja Mkuu.

vii) Kusimamia na kuhakikisha watumishi wote wa idara yake anawapangia majukumu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu husika kwa ufanisi.

viii) Kuandaa taarifa zote zitakazohitajika ikiwemo taarifa za mapato na matumizi kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na watumishi katika idara ya fedha.

ix) Kuandaa taarifa za kufunga hesabu za mwisho za mwaka wa Fedha ulioisha kwa kushirikisha na watumishi wa idara ya fedha pamoja na Meneja Mkuu.

x) Kuitisha na kuratibu vikao vyote vya watumishi wa idara ya fedha kwa kusikiliza changamoto zao, ushauri, mapendekezo na mambo kadha wa kadha yatakayojadiliwa.

xi) Kumshauri na kumsaidia Meneja Mkuu wa Kampuni katika masuala yote yahusuyo Fedha (Mapato na Matumizi)

xii) Atawajibika kutekeleza Majukumu mengine atakayopangiwa na Mwajiri.

**2.3. SIFA ZA MWOMBAJI.**

i). Awe na Shahada ya uhasibu au Stashahada ya juu ya uhasibu kutoka taasisi yoyote inayotambuliwa na serikali pamoja na cheti cha taaluma ya uhasibu CPA (T) au sifa inayolingana nayo inayotambuliwa na NBAA.

ii). Awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yenye kazi nyingi na kuzikamilisha bila kuathiri matokeo.

iii). Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) na kuendelea katika kazi za ufungaji wa hesabu za mwisho.

**2.4. MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMCM 1.**

**MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZILIZOTANGAZWA.**

i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.

ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.

iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.

v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".

vi. "Testimonials" "provisional results" "statement of result" hati matokeo za kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**

vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).

viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.

ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**

x. Ajira hizi ni za mkataba wa muda maalum.

xi. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia zifuatazo: Kwa njia ya Posta anuani ni

MENEJA MKUU,<br>
ARUSHA MEAT CO. LTD,<br>
S.L.P 14167,<br>
**ARUSHA-TANZANIA.**

*Au mwombaji atume maombi yake kupitia recruitment@arushameat.co.tz*

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **25/06/2025.**

***NB: Kwa wale waombaji ambao walishawasilisha maombi yao kupitia tangazo la awali kwa nafasi ya Meneja Fedha Na Mtunza Stoo hawatalazimika kuomba tena.***